# WARAKA WA PAULO KWA FILEMONI

1 Mimi Paulo, mfungwa kwa ajili ya Kristo
Yesu, na ndugu Timotheo, ninakuandikia wewe
Filemoni mpendwa, mfanyakazi mwenzetu
2 na kanisa linalokutana nyumbani kwako, na
wewe dada Afia, na askari mwenzetu Arkupo.
3 Tunawatakieni neema na amani kutoka kwa
Mungu Baba yetu, na kwa Bwana yesu Kristo.
4 Kila wakati ninaposali nakukumbuka wewe
Filemoni, na kumshukuru Mungu 5 maana
nasikia habari za imani yako kwa Bwana wetu
Yesu na upendo wako kwa watu wote wa Mungu.
6 Naomba ili imani hiyo unayoshiriki pamoja nasi
ikuwezeshe kuwa na ujuzi mkamilifu zaidi wa
baraka zote tunazopata katika kuungana kwetu
na Kristo. 7 Ndugu, upendo wako yameniletea
furaha kubwa na kunipa moyo sana! Nawe
umeichangamsha mioyo ya watu wa Mungu.
8 Kwa sababu hiyo, ningeweza, kwa uhodari
kabisa, nikiwa ndugu yako katika Kristo,
kukuamuru ufanye unachopaswa kufanya.
9 Lakini kwa sababu ya upendo, ni afadhali
zaidi nikuombe. Nafanya hivi ingawa mimi
ni Paulo, balozi wa Kristo Yesu, na sasa pia
mfungwa kwa ajili yake. 10 Basi, ninalo ombi
moja kwako kuhusu mwanangu Onesimo,
ambaye ni mwanangu katika Kristo kwani
nimekuwa baba yake nikiwa kifungoni. 11 Ni
Onesimo yuleyule ambaye wakati mmoja alikuwa

hakufai kitu, lakini sasa ananifaa mimi na wewe
pia. [12] Sasa namrudisha kwako, naye ni kama
moyo wangu mimi mwenyewe. [13] Ningependa
akae nami hapa anisaidie badala yako wakati
niwapo kifungoni kwa sababu ya Habari Njema.
[14] Lakini sitafanya chochote bila kibali chako.
Sipendi kukulazimisha unisaidie, kwani wema
wako unapaswa kutokana na hiari yako wewe
mwenyewe na si kwa kulazimika. [15] Labda
Onesimo aliondoka kwako kwa kitambo tu,
kusudi uweze tena kuwa naye daima. [16] Na sasa
yeye si mtumwa tu, ila ni bora zaidi ya mtumwa:
yeye ni ndugu yetu mpenzi. Na wa maana sana
kwangu mimi, na kwako atakuwa wa maana
zaidi kama mtumwa na kama ndugu katika
Bwana. [17] Basi, ikiwa wanitambua mimi kuwa
mwenzako, mpokee tena kama vile ungenipokea
mimi mwenyewe. [18] Kama alikuwa amekukosea
kitu, au alikuwa na deni lako, basi, unidai
mimi. [19] Naandika jambo hili kwa mkono wangu
mwenyewe: Mimi Paulo nitalipa! (Tena sina haja
ya kusema kwamba wewe unalo deni kwangu la
nafsi yako.) [20] Haya, basi, ndugu yangu, nifanyie
jambo hilo kwa ajili ya jina la Bwana; burudisha
moyo wangu kama ndugu katika Kristo.
[21] Naandika nikitumaini kwamba utanikubalia
ombi langu; tena najua kwamba utafanya hata
zaidi ya haya ninayokuomba. [22] Pamoja na hayo,
nitayarishie chumba kwani natumaini kwamba
kwa sala zenu, Mungu atanijalia niwatembeleeni.
[23] Epafra, mfungwa mwenzangu kwa ajili
ya Kristo Yesu, anakusalimu. [24] Nao akina
Marko, Aristarko, Dema na Luka, wafanyakazi

wenzangu, wanakusalimu. 25 Nawatakieni ninyi
nyote neema ya Bwana wetu Yesu Kristo.

# Biblia Takatifu
## Portions of the New Testament in the Swahili Language of Kenya, Mozambique, Somalia, and Tanzania, translation by Dr. Johann Ludvig Krapf completed in 1850

Public Domain

Language: Kiswahili (Swahili)

Dialect: Kimvita

Translation by: Dr. Johann Ludvig Krapf

2014-08-25

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 11 Nov 2022 from source files dated 9 Oct 2020
62071dc0-70e6-5b86-b569-c1b45e7771bd